



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA AFYA**

**BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA**

Tovuti: [www.hlpc.go.tz](http://www.hlpc.go.tz)



**TANGAZO**

**MAANDALIZI YA KUFANYA MITIHANI WA USAJILI**

Baraza la Wataalam wa Maabara linachukua nafasi hii kuwajulisha Wataalam wote kuwa maombi ya mitihani ya usajili yatakua yanafanyika kwa njia ya elektroniki kupitia mfumo HPRS.

Dirisha la maombi ya mitihani kupitia mfumo linategemewa kufunguliwa wiki ya pili ya Mwezi Machi 2023, Taarifa rasmi ya kufunguliwa kwa dirisha hili itatangazwa baadaye. Hivyo wataalam wanaotegemea kufanya mitihani wajiandae ili dirisha likifunguliwa waweze kufanya maombi na kukamilisha taratibu nyingine mapema bila kukwama. Dirisha la maombi ya mitihani litakua wazi kwa siku tano (5) mara baada ya kufunguliwa.

Wataalam wenye usajili wa awali (PRP) ambao waliupata nje ya mfumo wa [hprs.moh.go.tz](http://hprs.moh.go.tz) na wanaotarajia kufanya mitihani ya usajili ("First sit" au "Supplementary") watatakiwa kutuma ujumbe mfupi (SMS) kwenda namba **0734005777** ukiwa na; Majina Kamili, Barua pepe (e-mail), Namba ya usajili wa awali (PRP), Namba ya simu, Ngazi ya Elimu., Maneno "**USAJILI WA AWALI NJE YA HPRS**"

Kushindwa kutuma taarifa hizi kutasababisha kushindwa kufanya mitihani ya usajili na kuomba usajili wa kudumu

Zoezi la kupokea taarifa hizi **LITAFUNGWA RASMI 01.03.2023**

- Angalizo:**
1. Wenye usajili wa Kudumu hawahusiki na tangazo hili
  2. Tangazo hili haliwahuu wote wenye PRP ambazo waliomba kupitia mfumo
  3. Wale waliokwisha kutuma taarifa zao hawahusiki

Upatapo tangazo hili mtaarifu na mwenzako.

Imetolewa na Ofisi ya Msajili  
Baraza la Wataalam wa Maabara

